# INTERNATIONAL TEACHERS TRAINING COLLEGE

1013/2 MK

KISWAHILI

Mock 1

February 2020

## MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

## PRIMARY TEACHER EDUCATION

## KISWAHILI LUGHA
(Karatasi ya 2)

## MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

(SIRI)

Kijitabu hiki kina kurasa 12 zilizopigwa chapa

**USHAIRI: Abdilatif Abdalla :***Sauti ya Dhiki*
**Lililokuudhi ni lipi?**

1. (a) Tarbia - Lina mishororo minne kila ubeti.

Ukara - Vina vya kati vinalingana kiubeti tu wala sio katika shairi lote lakini vya nje vyote vimefanana katika beti za kwanza tatu ambavyo ni: ya- ya - ya - pi. Vina tamati vya ubeti wa mwisho ni ya-ya-ya na dhi

**Au**

Mathnawi - Lina vipande viwili kila mshororo.

**(Kutaja 1 na maelezo 1)**

(b) **Dhamira ya mwandishi:**

Iwapo mtu amekosewa asiweke mfundo bali amweleze aliyemkosea kile kilichomuudhi ili wapatane.

(1x2=2)

(c) Mshairi anasema huyo mpenzi wake hatendi sawa kwa kutowasiliana naye (i) kwani hatajua ni ubaya gani aliomfanyia yeye ambao umeleta yote hayo (ii). Yeye amewaza na halioni kosa lake (iii). Anasisitiza asimfiche au amweleze ni nini kilichomkasirisha. (iv).

( 4 x 1 = 4)

(d) **Muundo wa ubeti wa pili:**
Mathnawi – ubeti wa

(i) Ubeti una mishororo minne;

(ii) Ubeti una vipande viwili; ukwapi na utao

(iii) Mizani ni 8 kwenye ukwapi na 8 kwenye utao kila mshororo;

(iv) Vina vya kati na tamati ni - ko - ya;
ko - ya;
ko - ya;
ya - pi.

( 4 x 1 = 4)

| | | | |
|---|---|---|---|
| (e) sifundike | - | siweke moyoni | (1 x 1 = 1) |
| takisiri | - | kosa/ubaya | ( 1 x 1 = 1) |
| bui | - | rafiki/sahibu/mpenzi | ( 1 x 1 = 1) |

**TAMTHILIA: Jeff Mandila:** ***UPEPO WA MVUA***

**Jinsi mwandishi wa tamthilia ya *Upepo wa Mvua* alivyotumia mbinu ya nyimbo kukuza maudhui.** **(Alama 15)**

(a) Uk 2: Wimbo wa Kidani (ndotoni)

Wimbo huu unaonyesha kukosa matumaini. Hakuna chakutumaini au wa kumtumainia Watu maskini hawana pa kutafuta msaada.

Kutaja wimbo (Alama 1)
Kueleza maudhui (Alama 2)

(b) Uk 4: Wimbo wa Kidani (ndotoni)

Wimbo huu unaonyesha kukata tamaa katika maisha. Pia unaonyesha kutowajibika miongoni mwa viongozi.

Kutaja wimbo (Alama 1)
Kueleza maudhui (Alama 2)

(c) Uk. 65: Wimbo wa umati unaoandamana ukielekea kwa ofisi ya Chifu Mtoro. Wimbo huu unaonyesha maudhui ya mapinduzi/mageuzi dhidi ya uongozi dhalimu. Pia unaonyesha umoja na ushirikiano, utetezi wa haki na uamuzi dhabiti miongoni mwa wanyonge.

Kutaja wimbo (Alama 1)
Kueleza maudhui (Alama 2)

(d) Uk 69: Wimbo wa Kidani baada ya kukamatwa na askari wa Chifu Mtoro. Katika wimbo huu Kidani anamlaumu mama mzazi. Maudhui ya malezi yanabainishwa katika jamii. Pia unaonyesha ujasiri wa Kidani na mwanzo wa ukombozi.

Kutaja wimbo (Alama 1)
Kueleza maudhui (Alama 2)

(e) Uk. 74: Wimbo wa Amina baada ya kuelezwa na Waadi kuwa Kidani amekamatwa na kuteswa kwa kupigwa kisha kupelekwa hospitali. Wimbo huu unaonyesha matu maini. Pia unaonyesha imani.

Kutaja wimbo (Alama 1)
Kueleza maudhui (Alama 2)

(f) Uk.76: Wimbo wa Kidani baada ya kutoka hospitalini. Yumo nyumbani mwao. Wimbo huu unaonyesha ukosefu wa amani, ukosefu wa usalama, ukosefu wa ukweli (uongo unatawala) na pia unaonyesha dhuluma.

Kutaja wimbo (Alama 1)
Kueleza maudhui (Alama 2)

(g) Uk. 100: Wimbo wa Kidani. Anamwimbia ami yake Msa. Wimbo huu unaonyesha mapuuza, majuto, uzinduzi, kulaumu na kushawishi/kufikirisha.

| | |
|---|---|
| Kutaja wimbo | (Alama 1) |
| Kueleza maudhui | (Alama 2) |

2 (b) **Jinsi mwandishi wa tamthilia ya *Upepo wa Mvua* anavyojadili suala la uozo wa jamii.** **(Alama 15)**

(i) Uasherati - Waadi wa Bahati ni washerati.

(ii) Ulevi - Vijana wengi katika eneo la Bondeni ni walevi, kwa mfano Waadi na rafikiye.

(iii) Hongo - Chifu Mtoro anamhonga Pili ili amweleze mahali alipo Kidani.

(iv) Mauaji - Mhina aliuawa kwa sababu ya msimamo wake dhabiti.

(v) Uporaji wa mali ya umma - Watu wa Milimani walinyakua mashamba.

(vi) Ubadhirifu - Sengo anatumia karo ya shule kujiburudisha.

(vii) Ubinafsi/tamaa - Sengo anawaelekeza wanafunzi kwa shule yake ya kibinafsi.

(viii) Utovu wa nidhamu wa vijana kwa wazazi kwa mfano Waadi anamtusi mamake.

(ix) Utabaka - Watu wa milimani ni matajiri na ndio viongozi, wanaowadhulumu watu wa mabondeni.

(x) Matumizi mabaya ya mamlaka kwa mfano, Sengo.

(xi) Ukaragosi - Mtu I anakataa kushirikiana na wanamabondeni wenzake katika harakati za kujikomboa na kuusifu utawala dhalimu.

(xii) Usaliti - Askari I ni msaliti. Anaungana na raia kuupinga uongozi uliomwajiri.

(xiii) Mapuuza - Serikali kukosa kuwaelimisha wanamabondeni ilhali ni haki yao.

(xiv) Udikteta - Chifu Mtoro anajilazimisha uongozini kulingana na Kidani.

(xv) Ukatili - Kidani na Waadi wanachapwa hadi kuumizwa.

Hoja 15 x 1=15

RIWAYA: J. Habwe *Pendo la Karaha*

a) **Ukweli wa methali "Majuto ni Mjukuu" unavyodhainika kwa kurejelea wahusika wowote watatu katika riwaya ya *Pendo la Karaha.*** *(Alama 15)*

**Rehema**

Rehema ni wakala. Ni mama yake Kassim.

(i) Alijutia maisha mabaya aliyoishi mwanawe Kassim. Kassim alikula vya haramu, ni mlevi kupindukia na anatumia dawa za kulevya.

(ii) Alijutia kuwanadi watu. Aliwanadi wasichana wengi kwa mfano Rukia na Kudra kwa mataifa ya kigeni.

(iii) Alijutia kuvunja ndoa yake na mzee Choka, aliamua kumtafuta baadaye.

(iv) Alijutia kuitelekeza familia yake (Kassim na Choka).

(v) Alijutia kuthamini mali kuliko binadamu - alifahamu mateso waliyopitia wasichana aliowapeleka ughaibuni, lakini hakujali.

(vi) Anajutia kukataliwa na mwanawe kwa kukosa utu na kuishi maisha ya hali ya juu.

( Hoja 5x1 =5)

**Kudra**

(i) Anajuta kwa sababu ya fedheha zilizotokana na umaskini katika familia yake.

(ii) Anajuta kwa kufiwa na baba mzazi - babake aliuawa baada ya kufichua kashfa ya dawa za kulevya hapo Mombasa.

(iii) Anajutia tamaa yake ya kwenda ughaibuni hata baada ya Rukia kufia huko ughaibuni. Aliamua kwamba haendi hata akarudi shuleni kusoma.

(iv) Alijutia uamuzi wake wa kwenda Dubai alikokumbana na taabu nyingi k.m kupunguziwa mshahara na hata kufanya kazi katika ufuo.

( v) Alijutia kufanya mapenzi na mwajiri wake Salim kwa sababu alifutwa kazi baada ya bintiye Salim (Hanawi) kugundua. Chuki baina yake na Hanawi ilizuka kwa kuwa baba alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanawe.

(vi) Alijutia kumwibia mwajiri wake wa kwanza Bi Niyrat na Aminii pesa kwani jambo hili lilimhangaisha alipokuwa akitafutwa sana na polisi.

(vii) Anapopata matatizo huko Dubai anajuta kukaidi ushauri wa awali wa mamake kwamba asiende ughaibuni.

(Hoja 5x1 =5)

**Riziki**

(i) Anajutia umaskini katika familia yake.

(ii) Anajutia kitendo cha mumewe cha kufichua sakata ya dawa za kulevya jambo lililompelekea kuuawa.

(iii) Anajutia kumruhusu Kudra kwenda Dubai alikokumbana na matatizo mengi.

(iv) Anajutia kuwaajiri vijana waliomwibia baadaye na kuufilisisha mradi wa kuku.

(v) Anajutia kutamani maisha ya hali ya juu yaliyotokana na vijana waliokwenda kufanya kazi ughaibuni, jambo lililomfanya kuulegeza msimamo wa kumkataza Kudra kwenda Dubai.

(vi) Riziki anajutia kutoolewa kwa mwanawe Kudra.

3 (b).

(Hoja 5x1 =5)

(i) **Muktadha wa dondoo:**

**(Alama 5)**

(a) (i) Haya ni mawazo yanayompitikia Rehema akilini.

(ii) Alikuwa Bombolulu akimtafuta mwanawe Kassim.

(iii) Alimpata katika nyumba ya ajuza wake Zinduna.

(iv) Aliwaza haya baada ya Kassim kukataa kurejea nyumbani na kumkashifu kwa kunadi binadamu.

(Hoja 4 x 1= 4)

(ii) **Mbinu za lugha zilizotumika:**

(i) Uradidi/Takriri kwa mfano neno 'ulimwengu' limerudiwa.

(ii) Uzungumzi nafsia - dondoo hili ni maneno anayoyawaza Rehema mwenyewe na anajiwazia yeye.

(2 x 2 = 4)

(iii) **Umuhimu wa mzungumzaji katika ujenzi wa riwaya hii.**

Mwandishi amemtumia Rehema kukuza maudhui, wahusika na msuko katika riwaya. Maudhui yanayokuzwa ni:

(i) Kiburi - Alimfukuza mume wake kwa kujihisi amejitosheleza.

(ii) Utajiri usiofaa - Rehema ameshiriki biashara haramu ya kuwanadi wasichana.

(iii) Majuto - Anajutia kutelekeza familia yake na kushiriki biashara haramu.

(iv) Kuonyesha kuwa 'Mui huwa Mwema'. Rehema alibadilika na kuanza kuthamini familia na binadamu kwa jumla.

(v) Tamaa - Alitamani mali hadi kiwango cha kuwauza wasichana ughaibuni ili apate mali.

(vi) Uozo wa jamii - Rehema alinadi watu. Aidha alidharau mumewe na kuvunja ndoa yao.

(vii) Malezi mabaya - alimtelekeza mwanawe Kassim.

(viii) ametumiwa kuwajenga wahusika wengine kwa mfano kupitia kwake tunafahamu Mzee Choka ni mpole, na msamehevu.

(ix) anakuza migogoro ya wahusika riwayani kwa mfano, baina ya serikali na mawakala, baina ya waajiri ughaibuni na waajiriwa waafrika, migogoro katika ndoa n.k.

(x) Anakuza msuko kwa kujenga taharuki. Kwa mfano, anapojibidiisha kumtafuta mwanawe ili ampeleke 'rehab', je atafaulu?

Hoja 7 x 1 = alama 7)

4. **HADITHI FUPI**

(a) **Namna anwani *'Vazi la Mhudumu'* ni ilivyo jazanda.**

Mhudumu Daudi si 'mhudumu wa kweli'.

(i) Alianzisha kanisa ili kujinufaisha mwenyewe - ili kupata utajiri akisingizia kuwahudumia watu.

(ii) Alitumia ufadhili alioupata wa kuwasaidia watoto wanaorandaranda mitaani kujinunulia gari lake binafsi.

(iii) Alitumia kanisa kujitajirisha - alitumia juhudi za waumini za kuliendeleza kanisa ili kujinufaisha mwenyewe.

(iv) Alivaa vazi la mhudumu ili kujipatia wake za watu wengine kwa mfano Telila; pamoja na kuwafanyia miujiza ya watoto.

(v) Ingawa Daudi ni mhudumu, haheshimu cheo chake kwani anawahonga askari baada ya kupatikana na kosa la kwenda kwa kasi barabarani.

(vi) Hata hivyo, Daudi baada ya kupelekwa hospitali anapatikana na 'vazi' la kike - vazi la Telila

(vii) Daudi alikuwa mwongo kwani alipopatikana nyumbani kwa Telila alidai kuwa alikuwa ameitwa kwa maombi.

**Tanbihi:** Ingawa kwa kutazama nje hungeliona 'Vazi' hili, ndivyo ilivyo kuhusiana na maisha ya Daudi. Nje, Daudi ni mtumishi lakini ndani ni mwizi, fisadi, msherati, mchoyo, mdanganyifu. 'Vazi lilifunika maovu'.

Hoja 5 x 3 = 15)

4 (b) (i) **Umuhimu wa Mhusika Gretse katika hadithi ya *Aliua Mji wake* ya F. M. Sungula**

(i) Mhusika Gretse ametumiwa na mwandishi katika kukuza maudhui ya uwekezaji.

(ii) Pia anakuza maudhui ya uadilifu.

(iii) Aidha aliendeleza utangamano katika jamii.

(iv) Gretse anatoa ajira kwa watu mbalimbali.

(v) Gretse pia anakuza wahusika wengine kwa mfano Mwashumbe.

(vi) Mhusika Gretse ametumiwa kuonyesha mtu aliye na bidii katika kazi yake.

Hoja 5 x 1 = 5)

(ii) **Athari za ugaidi kwa mujibu wa hadithi ya *'Aliua Mji Wake'* (F. M. Sungula)**

(i) Unasababisha vifo vya jamaa.
(ii) Unaleta hali ya uyatima kwa mfano Musa, Rehema.
(iii) Unasababisha uharibifu wa mali.
(iv) Unasababisha ukosefu wa ajira.
(v) Unafanya watu wafungwe kwa mfano Musa na rafikiye wa kigeni.
(vi) Ndoto za kukamilisha elimu zinakatizwa kwa mfano ndoto ya Musa.
(vii) Unaleta majuto - Musa anajuta vitendo vyake.
(viii) Uchumi unaathirika - watalii wanarudi makwao.
(ix) Sifa ya nchi zinaharibika.
(x) Watu wanahama kwenda mahali kwingine kuliko salama.

Hoja 10 x 1= 10)

## SEHEMU YA B: MBINU ZA KUFUNDISHIA

5. **Mtahiniwa afuate hatua zifuatazo:**

(i) Utangulizi wa ngeli ya U-ZI.
(ii) Baadhi ya nomino ambazo hupatikana katika ngeli hii.
(iii) Wanafunzi wazitungie sentensi wakizingatia viambishi U-ZI (umoja na wingi).
(iv) Kueleza muundo wa kwanza - nomino zinazoanzia kwa herufi **'u'** katika umoja na **'ny'** katika wingi.
(v) Kutoa mifano ya nomino za muundo huu:

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Uzi | Nyuzi |
| Uta | Nyuta |

(vi) Kuwaongoza wanafunzi kutunga sentensi wakitumia nomino hizo.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Uzi umekatika | Nyuzi zimekatika |

(vii) Kueleza muundo wa nomino zinazoanzia kwa herufi **'u'** katika umoja na **'mb'** katika wingi.
(viii) Kutoa mifano ya nomino za muundo huo:

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Ubao | Mbao |
| Ubavu | Mbavu |

(ix) Kuwaongoza wanafunzi katika kutunga sentensi wakitumia nomino hizo.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Ubao umepatikana | Mbao zimepatikana |

(x) Kueleza nomino ambazo huchukua kiambishi **'u'** katika umoja na kiambishi **'nd'** katika wingi.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Ulimi | Ndimi |

(xi) Kutoa mifano ya sentensi wakitumia nomino hizo katika umoja na wingi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| [illegible] | Ndimi zimeumia |